



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE



Unapojibu tafadhali taja:

KUMB. NA. AC/18/214/49

Tarehe : 14/11/2022

## TANGAZO LA NAFASI ZA WAKUSANYA USHURU KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale anawatangazia Wananchi wa Wilaya ya Nyang'hwale nafasi za kazi. Hivyo, anakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi kama zilivyoainishwa katika tangazo hili.

### WANAOHITAJIKA

- ❖ Wakusanya Ushuru nafasi (10)

### MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kukusanya Ushuru katika eneo utakalopangiwa na Mwajiri
- ii. Kuhakikisha mapato yote ya Halmashauri yanakusanywa kwa kufuata taratibu
- iii. Kuhakikisha matumizi sahihi ya Mashine ya kukusanyia Ushuru (POS)
- iv. Kupeleka Benki fedha yote inayokusanywa kwa wakati

### SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe ni Mwananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale (Mkazi)
- ii. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne na kuendelea
- iii. Awe na Kitambulisho cha NIDA
- iv. Awe na afya njema, mwaminifu, mwenye kujituma
- v. Awe amepata Mafunzo ya mgambo


- vi. Mwombaji awe ni Mtanzania asiezidi umri wa miaka 45, awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale.
- vii. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa lolote la jinai, kufungwa jela au kupatikana na kosa lolote katika Utumishi wa Umma
- viii. Barua zote za maombi zipitie kwa Mshauri wa Mgambo Wilaya ya Nyang'hwale
- ix. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **18/11/2022 saa 9:30 alasiri**. Aidha maombi yote yawasilishwe kwa anuani ifuatayo

Mkurugenzi Mtendaji (W)

S. L.P 352

**NYANG'HWALE.**

Tangazo hili pia linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri [www.nyang'hwaledc.go.tz](http://www.nyang'hwaledc.go.tz) na katika mbao za matangazo.



Majagi R. Maiga

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
NYANG'HWALE.**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
S.L.P 352  
NYANG'HWALE**